

Methali za Hangaza (Tanzania)

**As Collected and Explained into Swahili
by Katekista Joseph Nkumbulwa**

**Compiled and Translated into English and into French
by Father Pascal Durand M. Afr.**

**Nairobi, Kenya: Privately Printed
February, 2011**

Methali za Hangaza (Tanzania)

Methali hizi zilikusanywa katika vijiji vifuatavyo: Mumuhamba, Lulemge, Bukililo, Kabanganga, Nyamiyaga, Sabajululigwa (Wilaya ya Ngara, hasa mpakani na Burundi). Baadhi ya Wahangaza waliosaidia kukusanya methali hizi ni Bonaventura Nzingo wa Kasiro na Mzingo Deus wa Lukole.

Uhangaza unakuwa kwenye wilaya ya Ngara. Unapakana na Ushubi na Uha (Kusini), Urundi (Magharabi), Uhaya (Kaskazini) na Wasubi (Mashariki).

Lugha ndugu za Kihangaza ni Kishubi na Kiha.

Wahangaza ni wachache sana, huenda hawazidi elfu hamsini. Kawaida ni wakulima na wawindaji. Chifu yao anaitwa Mwani (jina la cheo).

1. **Kihangaza**: Ilubuze inkwale ruvumbukana ikihuna.

Kiswahili: Kilichokosa kwale, hukulupusha bundi.

Maelezo: Kwale ni ndege anayetumiwa kama mboga katika maisha ya mwanadamu. Bundi ni ndege pia, ila haliwi bali anawaogofya wanadamu kwani ni mtumishi wa wachawi. Mwanadamu ajitahidi kutafuta mali, lakini tamaa yake ikizidi inaweza kumleta hasara. Pia, mwanadamu anayedharau faida ndogo kwa tamaa na mategemeo makubwa zaidi anaweza asiweze kupata chochote, mwishowe ni hasara tupu. Msemo mwingine kwa lugha ya kiswahili ni 'haraka haraka haina baraka', yaani haraka haraka hutenda yasiyostahili.

English: What will small birds overlook, the bigger ones will carry.

Français: (Petit à petit l'oiseau fait son nid).

2. **Kihangaza**: Ulusabira mukaaso lukatwala nyoko.

Kiswahili: Ukimwombea mabaya mama wa kambo, yanampata mama yako.

Maelezo: Usitake kumwombea jirani yako mabaya. Matokeo yake, ndugu yako anaweza akapata mabaya zaidi.

English: The ill you wished for your step-mother, your own mother receives.

Français: Le mal que tu désires pour ta mère nourricière, ta propre mère le reçoit. _

3. **Kihangaza**: Ulukwanu lukalula lukonhau mwana.

Kiswahili: Sungura akikua (akipata uzee) hunyonya mtoto.

Maelezo: Mzazi akikua, yaani akiwa na umri mkubwa wa uzee, hutegemea huduma na malezi kutoka kwa mtoto wake.

English: The old rabbit eats his child. The elders rely on the resources of their own children.

Français: Le vieux lapin mange sa progéniture. Les personnes, quand elles prennent de l'âge se reposent sur les ressources de leurs enfants.

4. **Kihangaza**: Akasozi kintahanugwa kahiye abagabo babona.

Kiswahili: Mlima usioshuriwa uliungua wanaume wakiangalia.

Maelezo: Mtu anayejifanya yeye ni mkubwa au tajiri katika jamii hataki ushauri kutoka kwa mwingine. Akipata matatizo jamii haiwezi kumsaidia inamwalia tu, kama jinsi kilima kinapowaka moto.

English: Mountains which do not welcome advises, got fire while people were simply watching. The proud people who claim to be self-sufficient were left alone in time of needs.

Français: La montagne qui ne reçoit pas de conseil, brûle alors que les gens ne font que regarder. L'homme fier qui est auto suffisant ne reçoit pas d'aide en temps de besoin

5. **Kihangaza:** Inkoko ilaye mwishamba bucha ya chiche inkwale.

Kiswahili: Kuku ikilala porini kukicha imekuwa kware.

Maelezo: Mwanamke au binti akianza matembezi ya kwenda kulala huko huyo tayari tabia yake imebadilika, yaani ameanza kuwa mjanja.

English: When the chicken starts to sleep in the bush, it has turned to be cunning. The woman or the girl which start to go out here and there has changed her habits and has become cunning.

Français : Quand la poule commence à dormir dans la brousse, elle est devenue maligne (pintade). Quand la femme ou la jeune fille sors ici ou la, ses habitudes sont toutes transformées et elle est devenue maligne.

6. **Kihangaza:** Ibikundanye bilajana.

Kiswahili: Vinavyopendana vinaenda pamoja.

Maelezo: Watu wanaoheshimiana hushirikiana kazi kwa pamoja bila manung'uniko.

English: Love unites and gathers. Respect and admiration for each other enables people to stay together in peace.

Français : Ceux qui s'aiment se retrouvent ensemble. (Ce qui se ressemble s'assemble). Le respect et l'admiration mutuelle permettent une vie commune paisible.

7. **Kihangaza:** Imienge yinzu imenywa nayo.

Kiswahili: Matundu ya nyumba huyafahamu mwenye nyumba.

Maelezo: Matatizo na shida ya kwenye mji huyafahamu kwa undani mwenye mji, usipende kupelezapeleza ya kwenye miji ya watu, bila kuombwa ushauri na uongo.

English: Holes in the house are known by the owner of the house. The inner troubles and difficulties are known best by insiders who do not need advises.

Français : Les trous dans la maison sont connus par le maître de maison. Les difficultés internes sont connus par les personnes habitants les lieux et ne peuvent en conséquence être facilement conseillées.

8. **Kihangaza:** Inkhoko isura heshi ntimenyaiyo yataye ilyoya.

Kiswahili: Kuku hufukuwa pengi hajui alikotupa unyoya.

Maelezo: Mtu hufanya kazi (biashara au kilimo) cha aina yoyote hajui atatajirikia kazi gani (juhudi).

English: The chicken which digs a lot does not know where it has left its feather. The person who works a lot does not loose.

Français : La poule qui fouille beaucoup ne sait pas à quel endroit elle a perdu sa plume. La personne qui travaille beaucoup ne perd pas.

9. **Kihangaza:** Infizi zibili aho zigwaniye ubwachi nibwa buhasigara.

Kiswahili: Mafahari mawili wanapogombana kinachoumia ni nyasi.

Maelezo: Mama na baba wanapogombana nyumbani wanaoathirika ni watoto. Pia viongozi wa serikali wanaposhindwa kuelewana, matokeo mabaya kwa waraia.

English: When two bulls fight against each other, the loser is the grass. When the chiefs are fighting against each other, the little ones are the greatest losers.

Français : Quand deux taureaux se battent entre eux, l'herbe est la grande perdante. Quand les chefs se querellent entre eux, les petits sont ceux qui perdent le plus.

10. **Kihangaza:** Nibilimo umunyu bilaseswa.

Kiswahili: Hata vyenye chumvi humwagwa.

Maelezo: Usifuate kila unachoona ni kizuri, ukifuata, mambo mengine yanapita tu. Dunia hii inapita na mambo yake mazuri.

English: Even what is salty is thrown away. Even what appears to be good and valuable pass away and therefore do not be attached to it.

Français : Même ce qui est salé se jette. Même ce qui apparaît comme précieux passe, il ne faut pas s’y attacher.

11. **Kihangaza:** Ulukundo gwumwana ruva kulinyina.

Kiswahili: Upendo wa mtoto unatokana na mama.

Maelezo: Malezi mazuri ya mzazi hata watoto huwa na tabia nzuri kwa jamii.

English: The love of a child comes from its mother. The good mother is the one causing a child to be good, out of her own goodness.

Français : La bonté d’un enfant vient de sa mère. Une mère bonne et généreuse est la vraie origine de la bonté et de la générosité de l’enfant.

12. **Kihangaza:** Aho utaye umwampi ukulikiza yo uundi.

Kiswahili: Unaponasa mshare unafuatiwa na mwingine.

Maelezo: Mtu anapopatia riziki, lazima kazi hiyo aipende, hata watu wengine wanaweza kumfuata.

English: When the arrow strikes, it is followed by another one. Let us love what we do and we will get followers.

Français : Quand la flèche atteint son but, elle est suivie par une autre. Aimons ce que nous faisons et le succès nous attirera des disciples.

13. **Kihangaza:** Inkoni ishikira igufa ntishikira ingeso.

Kiswahili: Fimbo hufikia mfupa haufikii tabia.

Maelezo: Mtoto unapomwadhibu kwa fimbo unaumiza mwili wake, huadhibu tabia wala hupigi tabia yake.

English: The stick which reaches the bone does not reach the behaviour. The hardness of the corporal discipline is not the best means to transform the behaviour of a child.

Français : Le bâton qui atteint l’os n’atteint pas le comportement. La dureté du châtiment corporel n’est pas le meilleur moyen de réformer un jeune.

14. **Kihangaza:** Hakulya limwe wodya kabili.

Kiswahili: Kuliko kula mara moja tu, afadhali kula mara mbili.

Maelezo: Unapoamua kufanya kazi ufanye kwa juhudi zote, bila kupiga uvivu.

English: Better than eating once is eating twice. When you decide to do something, to perform a special work, do it with all your capacity without laziness.

Français : Mieux vaut manger deux fois plutôt qu'une. Quand tu décides de faire quelque chose, fais le avec toute ta capacité sans fainéantise.

15. **Kihangaza:** Ubunda bunda abonwa nuhangaze.

Kiswahili: Anayenyemerea huonwa na aliyesimama.

Maelezo: Mtu anayefanya uovu akijidai haonekani lakini watu wanafahamu mienendo yake.

English: The person who boasts of his evil deed is seen by the standbayer. Even if he does not realise it, the morality of a person is known.

Français : La personne qui se vante du mal qu'il a commis est vue par le passant. Même si elle ne s'en rend pas compte, la moralité d'une personne est connue.

16. **Kihangaza:** Utitonze ntadya ibihiyle.

Kiswahili: Asiyevumilia hali vilivyoiva.

Maelezo: Mtu asiye na subira au uvimilivu hawezi kupata siri.

English: The person who is not patient cannot eat well cooked dishes. The person who has no discretion cannot be trusted with a secret.

Français : La personne impatiente ne peut pas manger de plats bien cuits. On ne peut confier de secret à la personne qui manque de discrétion.

17. **Kihangaza:** Iminsi ilasusa ntingana.

Kiswahili: Siku zinafanana lakini hazilingani.

Maelezo: Ingawa siku zote zina rangi moja, ukifanikisha katika kilimo mwaka huu, usitegemee na mwakani utafanyikisha. Hiyo ni mipango ya Mungu.

English: Days look alike but yet they are not the same. Perhaps you may think that next year you will get a harvest as good as the one of this year, but better put your trust in God.

Français : Les jours se ressemblent mais ne sont pas les mêmes. Peut-être seras-tu tenté de penser que l'an prochain tu auras une récolte aussi bonne que celle de cette année. Mieux vaut t'en remettre à la providence.

18. **Kihangaza:** Wanha kukulimila umwana wi nyoni uwawe ukahila.

Kiswahili: Unakataa kulimia mtoto wa ndege wa kwako, anakufa njaa.

Maelezo: Unashindwa kulima mpunga au mtama ukiogopa ndege wataumaliza, ukishindwa kutafuta mali ukiogopa wezi watakuiba na utakufa maskini, na utakuwa unatesa familia yako, siyo ndege wala mwezi.

English: When you refuse to cultivate because of fear of the birds (as they will eat your grain), then you prepare hunger for your own people.

Français : Quand tu refuses de cultiver par peur que les oiseaux viennent manger ton grain, tu prépares la famine pour ta propre maison.

19. **Kihangaza:** Ahari impene hasigaye ikiziriko.

Kiswahili: Palipokuwa mbuzi pamebakia kamba.

Maelezo: Palipokuwa pamefungwa mbuzi, mbuzi akifunguliwa hubaki kamba tu. Unapoahidiwa kupata kitu, unatakiwa kuwahi. Kukifuata ukichelewa unatakuta amepewa mwingine, utaambiwa kilikuwepo hapa lakini amechukuliwa na mwingine.

English: Where there was a goat, only the cord is left. When you are promised something, do not delay or you may lose it all.

Français : Là où il y avait une chèvre, il ne reste que la corde. Quand quelque chose t'est promis, ne retarde pas sinon tu risques de la perdre.

20. **Kihangaza:** Nta uvuga atayugishijwe.

Kiswahili: Hakuna anayesema bila kusemeshwa.

Maelezo: Hakuna mtu anayeweza kumchukia mtu bila kumkosea.

English: We cannot possibly say ill of another person without discrediting oneself. To speak ill of another person is to wrong him or her.

Français : On ne peut accuser quelqu'un sans se discréditer.

21. **Kihangaza**: Wankha kugaruka impeni ikirihafi ukabira nkhayo.

Kiswahili: Ukishindwa kuwarudisha mbuzi wakingari karibu utalia kama mbuzi.

Maelezo: Ukishindwa kuwalea watoto wako wakingali wadogo, watakapokuwa huwezi kuwadhhibiti matokeo yake, wewe mwenyewe watakusumbua.

English: Those who do not bring back the goats when they are close will be found crying like goats (in the attempt to call them back). Those who fail to educate well their children where they are young will suffer in their old age.

Français : Si tu ne ramènes pas les chèvres quand elles sont encore proches tu te trouveras en train de crier comme une chèvre. Ceux qui échouent à éduquer convenablement leurs enfants quand ils sont encore jeunes souffriront lors de leur vieillesse.

22. **Kihangaza**: Wankha kulima kule ukahasuma.

Kiswahili: Unakataa kulima mbali unalazimika kuhemea huko.

Maelezo: Kuna watu wanakataa kufanya kazi kwa mtu, matokeo yake anaenda kuomba msaada tena kwa huyo aliyekataa kufanya kazi kwake ili akulipe ajira.

English: If you refuse to work in a far away field, you will find yourself obliged to dwell there. If in your pride you refuse a work proposal from a neighbor of yours, you will find yourself coming back to him begging for help.

Français : Tu refuses de cultiver dans un champ éloigné, tu te trouveras obligé d'y résider. Si dans ta fierté, tu refuses une proposition de travail de la part d'un de tes voisins, tu te trouveras obligé de retourner chez lui en mendiant de l'aide.

23. **Kihangaza**: Ntauhora aho yabaye abayalahiliwe.

Kiswahili: Hakuna anayeishi alipozaliwa atakuwa amerizika.

Maelezo: Utakapozaliwa hata kama kwenye familia maskini ni lazima upe heshima.

English: Nobody is born satisfied. Do not disregard your family even if it is a poor one.

Français : Personne ne naît satisfait. Ne méprise pas ta famille, même si elle est pauvre.

24. **Kihangaza**: Ushaka kufa asomaingwe.

Kiswahili: Anayetaka kufa anabusu chumvi.

Maelezo: Mtu anayetafuta matatizo kama kifo kufungwa, anayeenda tofauti na jamii inavyoishi, kama vile kuwa mwizi.

English: Those who are desiring to die are kissing salt. Do not desire evil thing less it happens to you.

Français : Ceux qui désirent mourir embrassent le sel. Ne désire pas de choses mauvaises à moins qu'elles ne te surviennent.

25. **Kihangaza**: Impigi yambaligwa kuvura.

Kiswahili: Hirizi huvaliwa kwa kinga.

Maelezo: Unatakiwa kujikinga na kila uovu uliopo hapa duniani.

English: The fetishes are worn in order to prevent evil.

Français : Les amulettes sont portées par prévention. 'Mieux vaut prévenir que guérir'.

26. **Kihangaza**: Hakukomera wovyara.

Kiswahili: Kuliko kuwa na nguvu, bora uzae.

Maelezo: Ni bora kufanya kazi ili upate mali, kuliko kuwa na nguvu za kupigana.

English: Better than strength are children. Productivity in work is better than the mislead use of strength.

Français : Mieux vaut les enfants plutôt que la force. La productivité dans le travail est à preferer à un mauvais usage de la force.

27. **Kihangaza**: Umwana atinyaikara alikozeko.

Kiswahili: Mtoto anaogopa moto akishaungua.

Maelezo: Mtu anakuwa na tahadhari au wasiwasi kutomwamini mwingine aliyemwibia au kumdanganya.

English: Once bitten twice shy.

Français : Chat échaudé craint l'eau froide.

28. **Kihangaza**: Nta mwonga uburaisato.

Kiswahili: Hakuna mti unaokosa chatu.

Maelezo: Palipo na wingi wa watu hakosi mwenye tabia korofi. Kwenye miti, kuna miti na nyasi nyingi hawezi akakosa chatu.

English: There is no tree without a snake. When the people are numerous, there will be found somebody who is troublesome.

Français: Il n'y a pas d'arbre sans serpent. Quand les personnes sont nombreuses, on trouvera quelqu'un de dérangeant ou à la moralité douteuse.

29. **Kihangaza**: Ukunda ikitakukunda akaba alimvulaigwa mwishamba.

Kiswahili: Unapenda kisichopenda ni sawa na mvua inayonyesha porini.

Maelezo: Mvua haina hubaguzi, inanyesha kila mahali. Tunatakiwa tumtende haki kila mtu bila kuwa na ubaguzi.

English: To love those who are not loved is like the rain falling on the bush. The rain has no distinction as to where it falls, that is on the good and bad people alike. Likewise we should attempt to love everybody without discrimination.

Français: Aimer ceux qui ne le sont pas c'est comme la pluie tombant sur la brousse. La pluie ne distingue pas les bons des méchants quand elle tombe. De la même manière doit on s'efforcer de diriger nos intentions bienfaitantes sur tous sans discrimination.

30. **Kihangaza**: Ntautera ibuyeaho yatereche ikisabo.

Kiswahili: Hakuna anayeponda jiwe mahali alipoweka kibuyu.

Maelezo: Kibuyu ukikiponda kwa jiwe ni rahisi sana kuvunjika mahali ulipotunza kitu cha thamani siyo vizuri kupachezea.

English: We do not break stones into the earthenware pot. There is a need to choose the appropriate means for the projected purpose.

Français: On ne casse pas la pierre dans un pot en terre. Il faut prendre les moyens des buts que l'on se donne.

31. **Kihangaza**: Soo akwankha akuraga ivya munaniye.

Kiswahili: Baba asiyekupenda anakurithisha vilivyomshinda.

Maelezo: Baba asiyempenda mwanaye anamridhisha tabia ya chuki.

English: The father who does not love you gives you his failures. The father who does not love nor appreciate his child generates in him hatred.

Français: Le père qui n'aime pas son enfant lui transmet ses échecs. Le père qui n'aime pas son enfant génère en lui la haine.

32. **Kihangaza**: Icho utariye ubawibikiye.

Kiswahili: Ambacho haukukila umejitunzia.

Maelezo: Unapoacha kutumia mali katika anasa unatunzia urithi wa wanao au akiba yako ya baadaye.

English: What is not eaten today is kept for tomorrow. Invitation to prudence and foreseeing for the future.

Français: Ce qui n'est pas mangé aujourd'hui est gardé pour demain. Invitation à la prudence et prévoyance pour l'avenir.

33. **Kihangaza**: Iitaralenga ntulitele ingata.

Kiswahili: Kabla ya jua kuzama usikate tamaa.

Maelezo: Kupata mali hauna mwanzo au kikomo cha umri tafuta kwa muda wote wa maisha yako.

English: Before the sunset do not give up. There is no special time to succeed in life, so do not give up before the end of life.

Français: Avant le crépuscule, ne désespère pas. Il n'y a pas de temps spécial pour réussir dans la vie, aussi, il ne faut pas désespérer avant que la fin soit arrivée.

34. **Kihangaza**: Ibitahura ni misozi.

Kiswahili: Milima haikutani.

Maelezo: Unatakiwa kumtendea wema kila mtu. Unayekutana naye, ukimtendea vibaya ipo siku utakutana naye na utahitaji msaada wake.

English: Mountains do not meet. People meet again and again in life, unlike hills and mountains. Therefore do your best to stay in good relationships with everybody unless you regret afterwards.

Français : Les montagnes ne se rencontrent pas. Les personnes se rencontrent, à la différence des montagnes. Aussi faut-il s'efforcer de rester en bons termes avec tout le monde.

35. **Kihangaza**: Bukebuke nigwo rugendo.

Kiswahili: Pole pole ndiyo mwendo.

Maelezo: Tafuta mali kwa haki, utafanyikiwa tu.

English: Slowly is the way to succeed.

Français : Lentement est la manière de réussir. Petit à petit l'oiseau fait son nid.

36. **Kihangaza**: Uta inkhoko ntuta icho yabiche.

Kiswahili: Unatupa kuku hautupi alichowika.

Maelezo: Usimchukie mtu, chukia maneno yake machafu.

English: You do not throw away the hen with what it cried out. Do not reject the man, rather reject the evil he pronounced.

Français : Ne jette pas la poule avec son cri. Ne rejette pas l'homme, mais plutôt dénonce les paroles mauvaises qu'il a prononcé. (Jeter le bébé avec l'eau du bain).

37. **Kihangaza**: Umubindi ushira uvimye.

Kiswahili: Mtungwi hauwezi kujua panapokuwa pamejaa maji.

Maelezo: Mtu wa maji ukiwa umefunikwa huwezi ukautofautisha kuwa huu una maji au la. Huwezi ukajua tabia ya mtu kama hufahamiani naye au hujaishi naye.

English: The dugout canoe does not know the depth of the water. We cannot know the habits of a person unless we live with him or her.

Français : La pirogue ne connaît pas la profondeur de l'eau. Nous ne pouvons connaître les habitudes d'une personne à moins de vivre avec elle.

38. **Kihangaza**: Ukubaza kutera kumenya.

Kiswahili: Kuuliza kunasababisha kujua.

Maelezo: Usikubali kila jambo bila kuwa na maelezo yake.

English: To ask is to know. Asking questions is the way to acquire knowledge.

Français : Demander c'est savoir. Poser des questions est la manière de parvenir à la compréhension des choses.

39. **Kihangaza:** Umkwilima wisoni bamuhamba abona.

Kiswahili: Mkwilima mwenye aibu alizikwa huku akitazama.

Maelezo: Usione aibu kuuliza jambo hulijui, ukaamua kulifanya tu, mwisho wake kupata hasara.

English: The in-law who was ashamed has died in silence. Do not be timid to ask when you do not know, less you will fail and lose.

Français : Le beau-fils qui avait honte est mort en silence. Ne sois pas timide à demander quand tu ne connais pas, sinon cela pourrait causer ta perte.

40. **Kihangaza:** Umliolo yihebura yugaye.

Kiswahili: Maskini hukata tamaa akifunga.

Maelezo: Kuna watu wakitafuta mali kwa muda mrefu bila kupata mali, hukata tamaa.

English: The poor lost hope during his fast. Some people despair when they fail for too long.

Français : Le pauvre a désespéré lors de son jeûne. Certains perdent l'espoir quand ils échouent pendant trop longtemps.

41. **Kihangaza:** Ulutungu rulakula ntirusumba isozi.

Kiswahili: Bega haliwezi kuzidi shingo.

Maelezo: Mtoto hawezi akamzidi mzazi wake.

English: The shoulder is not higher than the neck. The child cannot surpass his or her parent.

Français : L'épaule n'est pas plus haute que le cou. L'enfant ne peut surpasser son parent.

42. **Kihangaza:** Umwana ahawe inyama yumutwe adyana nu kutwi.

Kiswahili: Mtoto akipewa nyama ya kichwa, hula na sikio.

Maelezo: Mtoto unavyomlea kwa tabia mbaya, hata wewe atageuka na kukudharau.

English: When the child is given meat of head piece meal, he eats even the ears. The child has no manner, therefore if he is not taught properly he will bring troubles.

Français : Quand on donne à l'enfant la viande provenant de la tête, il mange même les oreilles. Un enfant ne connaît pas les bonnes manières, alors s'il n'est pas éduqué convenablement, il sera source de troubles.

43. **Kihangaza:** Inchuti yu kuri iboneka muma gogwa.

Kiswahili: Rafiki wa kweli utamjua ukiwa na shida.

Maelezo: Rafiki au ndugu huweza kukujua wakati wa raha na shida.

English: It is when you are in difficulty that you will know who is really your friend (and also during happy times).

Français : C'est dans le besoin que l'on reconnaît ses amis (et aussi dans les moments heureux).

44. **Kihangaza:** Urufu nturubeshewa.

Kiswahili: Msiba hausingiziwe.

Maelezo: Siyo vizuri kusingizia una matatizo ili upate msaada.

English: We don't play with a death announcement. It is not wise to pretend you are in difficulty when it is not the case.

Français : Il ne faut pas prétendre une annonce de décès. Il ne convient pas de prétendre d'avoir des difficultés quand ce n'est pas vraiment le cas.

45. **Kihangaza:** Ukuri kucha muziko ntikusha.

Kiswahili: Ukweli hupita motoni bila kuungua.

Maelezo: Jambo lisilo la uongo (ukweli) watu hulipokea bila kuguna.

English: Truth crosses fire without getting burnt. When something is true, it is not affected by difficulties.

Français : La vérité traverse le feu sans être brûlée. La vérité ne saurait craindre les difficultés.

46. **Kihangaza**: Uwankha inyama yu mutwe akorakora wokwiwe.

Kiswahili: Anayekataa nyama ya kichwa ashike shike cha kwake ili aone kama kuna nyama.

Maelezo: Mtu anayekataa msaada kuwa ni kidogo ajiangalie yeye ana kitu gani.

English: The one who refuses to eat meat from the head piece, let him look what he owns in the first place. Let us not refuse help out of pride.

Français : La personne qui refuse la viande qui provient de la tête, qu'elle regarde ce qu'elle possède. Il ne faut pas refuser l'aide par fierté.

47. **Kihangaza**: Ntakibira kibura isato bababa taihize.

Kiswahili: Hakuna msitu unaokosa chatu.

Maelezo: Hakuna familia isiyo na mkuu wa kaya.

English: There is no forest without a snake (see number 28).

Français : Il n'y a pas de forêt sans serpent (voir numero 28).

48. **Kihangaza**: Inkhoko kazi ntibika ibayisema.

Kiswahili: Kuku jike hawiki na akiwika anajitakia ajali.

Maelezo: Kwa kawaida kuku jike hawiki, na akiwika lazima achinjwe. Mwanamke nyumbani hatakiwi kuwa na mamlaka ya kuzidi mamlaka wa Bwana yake.

English: The hen does not sing in the morning, and if it does, it looks for troubles. The housewife should remain under the leadership of her husband.

Français : La poule ne chante pas à l'aube, et si elle le fait, elle cherche son malheur. La femme au foyer doit reconnaître que la tête de la famille c'est le mari.

49. **Kihangaza**: Uwahushijwe ni nzoka yikanga umuserebayi.

Kiswahili: Aliyekoswakoswa na nyoka, hushituka aonapo mjusi.

Maelezo: Aliyepata ajali au hasara fulani kuwa na wasiwasi aonapo jambo lifananalo na lile alilolipata siku za nyuma.

English: The one who was confronted to a snake becomes afraid of the lezard. Once bitten twice shy.

Français : Celui qui a été confronté au serpent a peur du lézard. Chat échaudé craint l'eau froide.

50. **Kihangaza:** Ukiza umugwai wamaguru bukeye ngoingo twiruke.

Kiswahili: Ukimponya mgonjwa wa miguu utegemee atakuacha kwa mbio.

Maelezo: Mtu ukimsaidia katika matatizo mara nyingi usitegemee shukrani.

English: If you heal the leg of a person, do not be surprise if he uses to run away from you. When you help somebody, do not do it expecting thanksgivings.

Français : Quand tu guéris la jambe d'une personne, ne sois pas surpris qu'il l'utilise pour s'enfuir loin de toi. Quand tu offres ton aide, ne le fais pas en espérant une récompense.

51. **Kihangaza:** Urutoke rumwe ntirumena inda.

Kiswahili: Kidole kimoja hakivunji chawa.

Maelezo: Kazi ya mtu mmoja hilingani na kazi ya watu wawili wakishirikiana.

English: One finger does not kill the lice. Unity is strength.

Français : Un seul doigt ne tue pas la puce. L'union fait la force.

52. **Kihangaza:** Ugenda utabaza ukasaza utamenye.

Kiswahili: Asiyauliza hana ajifunzalo.

Maelezo: Unapojifunza kitu, lazima uulize. Sehemu ambayo huijui ili uweze kwenda kufanya kazi kwa uhakika.

English: The one who does not ask does not learn.

Français : Celui qui ne pose pas de questions n'apprend pas.

53. **Kihangaza:** Kibwiza ntushoboye kubuguzi ichokulya.

Kiswahili: Uzuri hauwezi kuufanya chakula.

Maelezo: Uzuri wa sura huwezi ukamkaribisha mtu kama uwezavyo kumkaribisha katika chakula usiwe na majivuno kwa sura au rangi yako.

English: Beauty does not produce food. Do not boast of the beauty of your face, be humble when welcoming.

Français : La beauté ne produit pas de nourriture. Ne te fie pas à la beauté du visage, plutôt, sois humble, serviable et accueillant en tout temps.

54. **Kihangaza:** Chwira nchwile ubulyohe mira mire umuliro.

Kiswahili: Tema niteme utamu meza nimeze moto.

Maelezo: Mtu mwenye tamaa, yeye anataka apate kila kitu, hata kama kuna matatizo anashindwa kukiacha kwa tamaa yake.

English: Desire makes you swallow fire. When somebody desires strongly something, he overlooks the difficulties in order to acquire it.

Français : Le désir te fait avaler le feu. Quand une personne désire de manière très grande, il ne soucie pas des difficultés afin qu'il obtienne l'objet de sa convoitise.

55. **Kihangaza:** Uwakutanze kukaraba niwe akutanga no kulya.

Kiswahili: Aliyekuwahi kunawa ndiye anayekuwahi kula.

Maelezo: Mtu anayeanza kulima ndiye atakayeanza kuvuna.

English: The one who comes first washing his hands is the one who will be first eating. The one who comes first to cultivate is the one who will be the first to harvest.

Français : Celui qui est le premier à se laver les mains sera le premier à manger. Celui qui est le premier dans les travaux de la culture sera le premier à la récolte.

56. **Kihangaza:** Umwungu ulyoshe waudya na ni nkondo.

Kiswahili: Boga tamu huliwa na maganda.

Maelezo: Mtu mwenye tabia nzuri, maneno yake yanalingana na sura yake.

English: A good vegetable is best eaten with its peel. When somebody is good, everything in this person is good, words and physical appearance.

- Français** : Une bonne légume se mange avec sa pelure. Quand quelqu'un est bon, tout dans cette personne est bon, ses paroles aussi bien que son apparence physique.
57. **Kihangaza**: Ichumu lya komerekeje umheshi.
- Kiswahili**: Mkuki ulimjeruhi mhunzi.
- Maelezo**: Matendo ya mtu humrudia kufuatana na tabia yake.
- English**: The spear has wounded the troublesome person. One should not play with fire.
- Français** : La lance a blessé celui qui faisait le malin. Il ne faut pas jouer avec le feu.
58. **Kihangaza**: umubumvi wi nkono alira murujo.
- Kiswahili**: Mfinyanzi wa vyungu hulua kwenye kigae.
- Maelezo**: Fundi hutengenezea wengine lakini yeye hajitengenezi, mkulima hulima na mwisho mazao yote huuzwa na yeye anabaki na njaa.
- English**: The potter eats in broken pots. Often, the farmer who produces food is the last one to enjoy the product of his work.
- Français** : Le potier mange dans des pots cassés. Les cordonniers sont toujours les plus mal chaussés.
59. **Kihangaza**: Umumezo mshasha utera amabavu.
- Kiswahili**: Mpini mpya husababisha matezi sugu mikononi.
- Maelezo**: Kitu kipya kuwa hakitoki rohoni kwani utakuwa bado unacho uchungu.
- English**: The new handle causes blisters in the hand. It takes time to be adjusted to something new.
- Français** : Le manche neuf cause des poulettes dans les mains. Il faut du temps afin de s'adapter a quelque chose de nouveau.
60. **Kihangaza**: Ukuseka kusumba kurila a.
- Kiswahili**: Aheri kucheka kuliko kulia.
- Maelezo**: Maisha mazuri ni yenye furaha kuliko yenye huzuni.

English: Better to laugh than to cry. Let us be optimistic.

Français : Mieux vaut en rire que d'en pleurer. Gardons l'optimisme.

61. **Kihangaza:** Utwisuka intarima nutwisuka niwabo.

Kiswahili: Asiyelima kwa kula ni wa kwanza.

Maelezo: Mtu mwongo ni mwepesi wa kujua kila jambo.

English: The one who does not cultivate is the first to eat. The liar is the first one to know anything.

Français : Celui qui ne cultive pas est le premier à manger. Le menteur est le premier à savoir ce qui se passe (il sait tirer les vers du nez).

62. **Kihangaza:** Akana kubwenge kamazekudya ngwi wachu barampamagaye.

Kiswahili: Mtoto mwenye akili, akimaliza kula kwenye mji anasema nyumbani wananiita.

Maelezo: Mtu anapokuwa kwenye starehe, ni vema kukumbuka kurudi kwake.

English: The wise child, when he has finished his meal at a neighbor's house says that he is called at his own home. When somebody enjoys a good time, he should remember to come back.

Français : Quand l'enfant sage a terminé son repas chez un voisin, il dit qu'il est appelé à retourner chez lui. Lorsque quelqu'un passe un bon moment, il doit se rappeler d'y mettre un terme et de revenir.

63. **Kihangaza:** Amagambo menshi gatera imvura kubura.

Kiswahili: Maneno mengi yanasababisha mvua kutonyesha na ukame.

Maelezo: Maneno wakati wa kazi husababisha kazi isifanyike. Uvivu huleta umaskini.

English: Many words cause the rain to stop. Too many words cause laziness, and laziness causes hunger and poverty.

Français : Trop de paroles empêchent la pluie de tomber. Trop de paroles sont la cause de négligence dans les travaux, et par conséquent de famine et de pauvreté.

64. **Kihangaza**: Imvura ili kure nti kunyagira.

Kiswahili: Mvua iliyo mbali haikunyeshei.

Maelezo: Jambo lisilokuhusu haliwezi kukudhuru.

English: The far away rain does not reach you. A matter which does not concern you does not affect you.

Français : La pluie lointaine ne t'atteint pas. Une chose qui ne te concerne pas ne saurait t'affecter.

65. **Kihangaza**: Ntiwishime utarashinda.

Kiswahili: Usijisifu kabla hujashinda.

Maelezo: Ukiwa hapo duniani usiwe na majivuno mbele ya watu.

English: Do not boast before the victory.

Français : Ne fais pas le fier avant la victoire. (Rien ne sert de courir, il faut partir à point ou vendre la peau de l'ours avant de l'avoir tué).

66. **Kihangaza**: Inzoka iligorola ikaba ihise.

Kiswahili: Nyoka akijinyosha ameondoka.

Maelezo: Mtu akiondoka mkingali maongezi naye uelewe amedharau maongezi yako.

English: The serpent has left straightening itself. When somebody suddenly leaves you while lifting up his head, know that he has despised your own words.

Français : Le serpent a quitté en se raidissant. Quand une personne te quitte soudainement la tête haute, sache qu'il a méprisé tes paroles.

67. **Kihangaza**: Umuntu wingeso nziza adya nicha nyegejwe.

Kiswahili: Mtu mwenye tabia nzuri anakula hata kilichofichwa.

Maelezo: Ukiwa na tabia nzuri ni rahisi kupewa siri.

English: A good mannered person eat even what is hidden. Somebody who has good manners easily receives secrets.

Français : La personne bien éduquée mange même ce qui est caché. Une personne qui a de bonnes manières facilement on lui confie des secrets.

68. **Kihangaza**: Umudaho ntudaha muundi.

Kiswahili: Kata haichoti ndani ya kata nyingine.

Maelezo: Huwezi kuingilia mambo ya ukoo mwingine.

English: A family does not take from another family. We cannot interfere into the matters of another clan.

Français : Une famille ne puise pas dans une autre famille. Nous ne devons pas interférer dans les affaires d'un autre clan.

69. **Kihangaza**: Inzovu ninanigwa umutonzi.

Kiswahili: Tembo hashindwi mkonga wake.

Maelezo: Mzazi hashindwi kumlea mtoto wake au kila mmoja ana uwezo wa kukabiliana na jambo linalomtokea.

English: The elephant does fail to care for his trump. Parents can not fail to care for their children. What is necessary for this task is already given to them.

Français : L'éléphant n'est pas embarrassé de sa trompe. Le parent ne saurait échouer à élever convenablement son enfant. Ce qui lui est nécessaire pour parfaire cette tâche lui est déjà donné d'avance.

70. **Kihangaza**: Umunurati yahuye ni bichu.

Kiswahili: Mtengeneza mvua alikutana na mawingu.

Maelezo: Kumtafuta mtu na unakutana naye.

English: The rain-making person has been met under the clouds. You were looking or talking about somebody, and here it is that you are meeting him.

Français : Celui qui fait tomber la pluie a été rencontré alors que le temps était nuageux. Tu cherchais ou parlais au sujet de quelqu'un et voici que tu le rencontres. Il suffit de parler du loup pour en voir la queue.

71. **Kihangaza**: Umuntu wese agira ibanga dyiwe.

Kiswahili: Kila mtu ana siri yake.

Maelezo: Mtu mwenye akili timamu hutunza siri.

English: Each one has his own secret. A good person knows how to protect his secrets.

Français : Chaque personne possède son propre secret. Une personne adulte sait comment garder ses secrets.

72. **Kihangaza:** Umpumwi yabonye ukwezi.

Kiswahili: Kipofu aliona mwezi.

Maelezo: Mtu asiyejua akifahamu jambo, hulitangaza kwa kila mtu.

English: The blind person has seen the moon. The one who does not usually know, when he comes to know something tends to proclaim it everywhere.

Français : L'aveugle a vu la lune. La personne qui habituellement vit dans l'ignorance, si elle parvient à connaître quelque chose, tend à la proclamer partout.

73. **Kihangaza:** Umuntu yi yaga aho ageza uboko.

Kiswahili: Mtu hujikuna anapofikisha mkono.

Maelezo: Kila mtu afanye jambo kazi kulingana na uwezo wake.

English: In order to scratch yourself you have to stretch your arm. Each should work according to his capacity.

Français : Pour se gratter, il faut étendre le bras. Chacun doit travailler selon ses capacités. (Avoir les yeux plus grands que le ventre).

74. **Kihangaza:** Ufise akabi kumubiri icho ukoze chose nturonkha.

Kiswahili: Ukiwa na mkosi kila unachotafuta haufanikishi.

Maelezo: Unatakiwa ujuwe unaishi namna gani na jamii.

English: If you are with somebody holding grudges against you, you will not succeed in whatever you do. You must know how and with which kind of people you are living with.

Français : Lorsque tu te trouves avec quelqu'un qui tient quelque chose contre toi, tu ne saurais réussir. Il est nécessaire de savoir comment et avec quel genre de personne tu te situes.

75. **Kihangaza**: Kwiruka na urukwavu ino uliko uraseka.

Kiswahili: Kukimbiza huku unacheka.

Maelezo: Sungura ni mkimbiaji sana, huwezi kumkimbilia ukiwa unacheka. Unapofanya kazi, lazima uache mzaha ili uweze kufanikiwa.

English: To run after somebody while laughing. When you are performing a particular task, put your whole self into it in order to succeed, do not take it lightly.

Français : Poursuivre quelqu'un en riant. Quand tu fais un travail particulier, mets-y tout ton cœur afin de réussir, ne prends pas cette tâche légèrement.

76. **Kihangaza**: Basangira inzoga ntibasangila umugole.

Kiswahili: Wanaochangia pombe siyo mwanamke.

Maelezo: Kuna kitu cha kuwa na mtu peke yake kama mke na Bwana (usizini).

English: Women do not contribute for beer. Sometimes it is necessary to respect privacy.

Français : Le femmes ne contribuent pas pour la bière. Il faut savoir parfois faire respecter les affaires privées.

77. **Kihangaza**: Nakataroza mzokazana.

Kiswahili: Ubaya huletwa na utundu.

Maelezo: Mtu mwenye tabia mbaya au kuonekana hafai kwa watu hutokana na tabia yake.

English: Badness comes from bad manners. Somebody who has evil intentions will be known by his bad manners.

Français : La mauvaiseté provient des mauvaises manières. La personne ayant des intentions mauvaises se laissera deviner par ses propres manières.

78. **Kihangaza**: Uhunira chane ukimbura ingonera.

Kiswahili: Ukisinzia sana utavuna tongotongo.

Maelezo: Mtu anapokuwa usingizini hafanyi kazi lakini hupata tongotongo, hazina faida kwake. Mtu anapopiga uvuvi matokeo yake huwa fukara.

English: If you forget yourself, you will reap pea-nuts. Laziness begets poverty.

Français : Si tu t'oublies, tu ne récolteras que des cacahuètes. La paresse génère la pauvreté.

79. **Kihangaza:** Utarika munda ukatarula ivyoboze.

Kiswahili: Ukivundika tumboni utatoa vilivyoza.

Maelezo: Huwezi ukaweka akiba kwenye tumbo, kwa kula. Unatakiwa kutunza mali ili iweze kukusaidia siku za mbele.

English: Enlarge your stomach and you will be left only with what is rotten. It is not possible to store in the stomach. It is necessary to store in some proper place in order to survive days ahead.

Français : Enfle l'estomac et tu n'auras que du pourri. Il n'est pas possible de mettre les réserves dans l'estomac. Il est donc nécessaire d'engranger dans un endroit approprié pour survivre les jours à venir.

80. **Kihangaza:** Ntuuhora ahiliwe.

Kiswahili: Hakuna anayekaa na furaha siku zote.

Maelezo: Katika maisha ya mwanadamu, yamejaa matatizo.

English: It is not possible to remain happy always. Accept the troubled times just as you welcomed the happy moments.

Français : Personne ne peut rester heureux tout le temps. Accepte les mauvais moments juste comme tu as accueilli les moments de bonheur.

81. **Kihangaza:** Impuzu yokutiira ngo tamba ntuntaburile.

Kiswahili: Nguo ya kuazima cheza usinipasulie

Maelezo: Kitu cha kuazima tumia ila usikiharibu.

English: The cloath that you borrowed, use it but do not spoil it. Care carefully for the tool you requested for a time.

Français : L'habit qu'on te prête, utilise-le mais ne le déchire pas. Fais attention aux outils que le voisin te prête.

82. **Kihangaza:** Intungo dyu mworo ntiliramba.

Kiswahili: Mfugo wa maskini haudumu.

Maelezo: Mawazo ya maskini hayasikilizwi.

English: The cattle of the poor does not last. The poor man rarely succeeds, and the ideas of the poor person are not listened to.

Français : Le troupeau du pauvre ne dure pas. Les idées du pauvre ne sont pas écoutées.

83. **Kihangaza:** Uubuze kwagira abayakubonye.

Kiswahili: Anayekosa la kufanya hana jinsi.

Maelezo: Mtu asiyefanya kazi huweza kudharau kila kazi ya mtu, kwani yeye hana uwezo wa kuifanya.

English: The lazy one is always wrong. The person who does not work can not find arguments to defend one self.

Français : Le paresseux a toujours tort. La personne qui ne travaille pas ne peut trouver d'arguments pour se défendre.

84. **Kihangaza:** Inzovu yichwa nu runyegeri.

Kiswahili: Tembo huuwawa na sisimizi.

Maelezo: Mtu mdogo anaweza kumshauri jambo zito hata mkubwa. Husidharau jambo lolote.

English: The aunts have killed the elephant. Even the smallest person can provide a salutary advice.

Français : Les fourmis ont tué l'éléphant. On a toujours besoin d'un plus petit que soi.

85. **Kihangaza:** Imbwa ntikuga ichoitabonye.

Kiswahili: Mbwa habweki bila kuona kitu.

Maelezo: Mtu humchukia mtu aliyemfanyia jambo baya.

English: the dog doe not bark if it has not seen anyone. Grudges come because of some wrongdoings.

Français : Le chien n’aboie pas s’il n’a vu personne. L’inimitié provient de quelque mauvaise actions. Il n’y a pas de fumée sans feu.

86. **Kihangaza**: Uugiye ntagirango ndaje.

Kiswahili: Aliyekwenda hasemi.

Maelezo: Mtu alyekufa haagi.

English: The one who went away does not bid farewell. The person who died did not say bye.

Français : Celui qui est parti n’a rien dit. La personne décédée n’a pas dit ses adieux.

87. **Kihangaza**: Hashimaumutina nihashimainda.

Kiswahili: Moyo ndiyo unaoshukuru.

Maelezo: Tumbo halishukuru, binadamu akipewa kitu hushukuru lakini huzidi tena kuomba na kukiona alichopewa hakitoshi.

English: The heart is the one who is grateful. The belly does not say thank you as it always needs again and again. Only the heart of a person can be truly grateful.

Français : Le reconnaissant, c’est le coeur. Le ventre ne sait pas dire merci car il a toujours besoin de davantage. Seulement le coeur d’une personne sait être vraiment reconnaissant.

88. **Kihangaza**: Umpe nkuroge unyime kuroge.

Kiswahili: Unipe nikuloge, uniuime nikuloge.

Maelezo: Kuna watu husaidiwa lakini huzidi kulaumu tu. Umsaidie usimsaidie yeye ni majungu tu.

English: Give me so that I bewitch you, hurt me so that I bewitch you. Some people would never be satisfied but will find grudges no matter what is done to them, whether good things or bad things.

Français : Donne-moi afin que je t’ensorcelle, fais-moi du mal afin que je t’ensorcelle. Certaines personnes ne sont jamais satisfaites mais cherchent noises quoique l’on fasse pour eux.

89. **Kihangaza**: Ntuseke inzoga yu mubayi nawe wanchwe uburo.

Kiswahili: Usicheke pombe ya jirani nawe umeanika ulezi.

Maelezo: Mwenzako anapopata matatizo usimcheke, bali umpatie faraja kwani matatizo ni kwa wote hata wewe unaweza kuyapata.

English: Do not laugh about the beer of your neighbour while you just spread your millet under the sun. When your neighbour got some problems, do not despise him but instead, try to console him as what he has suffered you may get it as well.

Français : Ne te moque pas de la bière de ton voisin alors que ton mil est encore au soleil. Ne te moque pas du malheur de ton voisin, mais plutôt, cherche à le consoler. Ce qui lui est arrivé, cela peut te parvenir également.

90. **Kihangaza:** Udye bike ulyame kare.

Kiswahili: Kula kidogo ulale mapema.

Maelezo: Katika maisha ya binadamu hapa duniani, anatakiwa awe na kiasi ili awezi kuishi kwa raha.

English: Eat little and sleep early. Be with measure in everything.

Français : Mange peu et dors tôt. Use de mesure en toute chose.

91. **Kihangaza:** Umuhizi yakunze umulilo.

Kiswahili: Mwindaji aliyependa moto.

Maelezo: Mtu anayependa starehe hufanikiwi, hapati mali kwani muda mwingi kutofanya kazi.

English: The hunter who loves fire. The person who loves too much feasting cannot hope to succeed as he wastes his time.

Français : Le chasseur qui aime le feu. La personne qui aime trop les festivités ne peut espérer réussir puisqu'elle gaspille son temps.

92. **Kihangaza:** Uwichaye kuntebe niwe mwami.

Kiswahili: Aliyekalia kiti ndiye mtawala.

Maelezo: Mtu aliye na mali ndiye anayesikilizwa, mara nyingi kuliko maskini.

English: The one who is sitting on the throne, this is the leader. The man with wealth is the one who is listened to.

Français : Celui qui est assis sur le trône, c'est celui qui préside. La personne riche est celle qui est écoutée.

93. **Kihangaza**: Uwarushe ntaruhuka.

Kiswahili: Aliyechoka hapumziki.

Maelezo: Mtu anayefanya kazi kwa juhudi huipenda kazi yake, mtu akipata matatizo lazima ayakubali ili aweze kuyatatua.

English: The one who is tired does not rest. The one who likes his work does not stop easily, however he has to take some distance from his work in order to find solutions to some difficulties.

Français : Celui qui est fatigué ne se repose pas. La personne qui aime son travail ne s'arrête pas facilement. Cependant elle doit prendre de la distance par rapport à son travail afin de trouver des solutions à ses problèmes.

94. **Kihangaza**: Nase kulila mawe umfu kunuma.

Kiswahili: Hata aliliaye mamaye mfu hunyamaza.

Maelezo: Mtu anapopata matatizo anatakiwa kujifariji.

English: Even the dead shut up in front of the one crying for his mother. In front of hardships, people are entitled to be consoled.

Français : Même le mort se tait devant celui qui pleure sa mère. Devant la souffrance, la personne humaine doit être consolée.

95. **Kihangaza**: Umubi mgenzi kukwila byosi nacho biza.

Kiswahili: Ubaya wa mtu huenea zaidi kuliko uzuri.

Maelezo: Mtu mwenye tabia mbaya mfano mwizi, kila akitapo watu humsema vibaya.

English: The wrongdoings of a person spread more than his goodness. Human beings are more eager to blame than to praise.

Français : Les mauvaises actions d'une personne courent plus vite que sa bonté. Les humains sont davantage portés à condamner plutôt qu'à louer. (Le bruit ne fait pas de bien et le bien ne fait pas de bruit, Saint François de Sales).

96. **Kihangaza**: Alipendekeza mmela ekibi.

Kiswahili: Anayejipendekeza mwisho huharibu.

Maelezo: Mtu anayejifanya kufahamu kila jambo matokeo yake kuharibu.

English: The proud person will destroy himself. The person who claims to know everything is running to his loss.

Français : Le prétentieux court à sa perte. La personne qui prétend tout connaître ne peut durer sans se perdre.

97. **Kihangaza:** Hugile huchachane hugile enzigo.

Kiswahili: Ukiwa mlafi usiwe mchoyo.

Maelezo: Ukipenda kupokea ya wenzako lazima nawe utoe ya kwako.

English: If you are glutton, don't be greedy. If you like to eat your neighbour's you have to give at your turn.

Français : Le glouton ne doit pas être pingre. Si tu aimes profiter de l'aide du voisin, souviens-toi que le jour viendra où il te faudra donner à ton tour.

98. **Kihangaza:** Umkuza wana nenzoga lulimi vishi.

Kiswahili: Kibuyu cha pombe hulegeza ndimi nyingi.

Maelezo: Mnywaji wa pombe anapolewa hutoa maneno kinywani mwake bila utaratibu.

English: The beer pot untie many tongues. The person who drunk too much speaks many words without control.

Français : Le pot de bière délie bien des langues. La personne qui a trop bu ne peut contrôler ses paroles.

99. **Kihangaza:** Inkingi ifata inzu ntiha naguligwako inzoga.

Kiswahili: Nguzo kuu ya nyumba haipanguswi pombe.

Maelezo: Mzazi na mzazi tu, hutakiwi kumdharau.

English: The great piece of cloth from the house does not wipe the bear. The parent ought not to be despised.

Français : Le grand linge de maison n'essuie pas la bière. Le parent ne doit pas être méprisé.

100. **Kihangaza**: Engezo niviza mnebye mkozi.

Kiswahili: Mlafi daima ni mvivu wa kazi.

Maelezo: Mtu asiyepeleka kufanya kazi daima hupenda kupata kila kitu.

English: The glutton is always a lazy person. The person who is lazy does not like to profit from others.

Français: Le glouton est toujours paresseux. La personne paresseuse aime profiter des autres.

101. **Kihangaza**: Inda yaha nohusubila kulya.

Kiswahili: Tumbo lililoshiba halilijui lisiloshiba.

Maelezo: Mtu tajiri hamthamini mtu maskini.

English: The satisfied stomach does not know the empty belly. The wealthy person does not value the poor.

Français: Le ventre plein ne connaît pas l'estomac vide. La personne riche ne porte pas d'estime envers la personne pauvre.

102. **Kihangaza**: Wammaye kitoke injewe ulampaye mkuyu.

Kiswahili: Nimekupa mgomba, wewe ukanipa mkuyu.

Maelezo: Nimekupatia kitu cha faida, wewe ukanirudishia matusi.

English: I gave you a banana tree and you gave me a baobab. While I gave you something valuable you responded by giving back something useless.

Français: Je t'ai donné un pied de bananes et tu me rends un baobab. Alors que je t'ai confié quelque chose de valeur, tu me rends quelque chose inutile.